



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
MAENDELEO YA VIJANA
S.L.P. 2255, DODOMA



TANGAZO KWA UMMA

NAFASI ZA WAJUMBE VIJANA WA TAIFA KATIKA JUMUIYA YA MADOLA

Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana inawatangazia vijana wa Kitanzania nafasi mbili (2) za Wajumbe Vijana wa Taifa katika Jumuiya ya Madola, yaani mwanamke mmoja na mwanamume mmoja, watakaohudumu kwa kipindi cha miaka miwili. Wajumbe hao watawakilisha vijana wa Tanzania katika Jukwaa la Vijana linalofanyika sambamba na Mkutano wa Wakuu wa Serikali wa Jumuiya ya Madola (CHOGM 2026), utakaofanyika tarehe 1 hadi 4 Novemba 2026, St John's, Antigua na Barbuda, pamoja na shughuli nyingine za Jumuiya hiyo.

Sifa za mwombaji:

- Awe raia wa Tanzania;
- Awe na umri wa miaka 18 hadi 29;
- Awe na uelewa wa sera, mikakati, fursa na changamoto za vijana nchini;
- Awe na uzoefu katika shughuli za maendeleo ya vijana, uongozi au kujitolea katika jamii;
- Awe na uwezo mzuri wa mawasiliano kwa Kiswahili na Kiingereza; na
- Awe tayari kuhudumu kwa miaka miwili na kusafiri ndani na nje ya nchi.

Namna ya kuomba:

Mwombaji anatakiwa kuwasilisha:

1. Barua ya maombi; na
2. Wasifu binafsi (CV).

Maombi yatumwe kwa: **Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana, S.L.P. 2255, Dodoma**, au kwa barua pepe: bestina.gunje@vijana.go.tz. Nakala kwa nassibu.mwaifunga@vijana.go.tz.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20 Oktoba 2026.

Vijana wa jinsia zote wanahimizwa kuomba. Waombaji watakaokidhi vigezo ndio watakaowasiliana nao kwa ajili ya usaili.

Tangazo hili linapatikana pia kwenye Mfumo wa YES na tovuti ya Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana, Dodoma